# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI
## OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

## MHESHIMIWA DKT. SAADA MKUYA SALUM (MBM)
## KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI
## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**MEI, 2021**



**Mhe. Othman Masoud Othman**
**Makamu wa Kwanza wa Rais - Zanzibar**



**Dkt. Saada Mkuya Salum**
**Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Zanzibar**



**Bi Khadija Khamis Rajab**
**Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Zanzibar**

YALIYOMO

A.UTANGULIZI....................................................................................1
B.MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021..............................................4
MAPATO..........................................................................................4
MATUMIZI......................................................................................4
UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2020/2021.............5
B01 OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS.......................5
i.Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ......................................................................5
ii.Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu...8
iii.Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi ......................................................10
C04 – TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA – PROGRAMU YA UDHIBITI WA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA DAWA ZA KULEVYA......................................................13
CO5 - TUME YA UKIMWI - PROGRAMU YA KURATIBUMWITIKO WA TAIFA WA UKIMWI ............16
C. MUELEKEO WA PROGRAMU ZA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 .....................................................................................19
B01 – OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS..................21
i.Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ...................................................................22
ii.Programu ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi...............................23
iii.Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu........................................................................... 23

iv.Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi ....................................................24
C04 – TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA – PROGRAMU YA UDHIBITI WA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA DAWA ZA KULEVYA ........................................................ 26
C05 – TUME YA UKIMWI - PROGRAMU YA KURATIBU MWITIKO WA TAIFA WA UKIMWI ............................ 27
D.SHUKURANI ..................................................................................28
E.HITIMISHO.....................................................................................30
Kiambatanisho nam. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha Julai 2020 - Machi 2021 (000) ................................................... 32
Kiambatanisho nam. 2: Muelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 (000) ............................................................... 35
Kiambatanisho nam. 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai-Machi 2020/2021na Makadirio ya 2021/2022 .......................37
Kiambatanisho nam. 4: Miradi ya Maendeleo Inayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ....................................... 38
Kiambatanisho nam. 5: Maeneo Yaliofanyiwa Ufuatiliaji wa Kimazingira ..................................................................... 43
Kiambatanisho nam. 6: Miradi Iliyofanyiwa Tathmini za Kimazingira ......................................................................................... 45
Kiambatanisho nam. 7: Miradi ya Kiuchumi na Kimaendeleo Iliyofanyiwa Ufuatiliaji wa Kimazingira ......................................... 50
Kiambatanisho Nam. 8: Taarifa za Malalamiko ya Kimazingira Zilizopokelewa na Kushughulikiwa ................................................. 54
Kiambatanisho Nam. 9: Idadi na Aina ya Vipindi vya Redio na TV vilivyotayarishwa ......................................................... 63

Kiambatanisho Nam. 10: Mchanganuo wa Wanufaika wa Mfuko waMaendeleo ya Watu Wenye Ulemavu ............................ 65
Kiambatanisho Nam. 11 Idadi ya Wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ............................................................ 66
Kiambatanisho Nam. 12: Stahiki za Wafanyakazi .......................... 69
Kimbatanisho Nam. 13: Idadi ya Watumishi Waliopatiwa Mafunzo ............................................................................................ 70

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI
## OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

## MHESHIMIWA DKT. SAADA MKUYA SALUM (MBM)
## KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI
## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia kukutana ili kujadili utekelezaji wa majukumu yetu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2021/2022. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, natoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuliongoza vyema Taifa letu. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua zake anazochukua za kuipeleka Zanzibar katika maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii. Kasi yake kubwa aliyoanza nayo ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 inatoa muelekeo kuwa Zanzibar itapiga hatua kubwa ya maendeleo makubwa katika

kipindi kifupi kijacho. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuongoze vyema Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake.

3. **Mheshimiwa Spika,** ninachukua fursa hii kumpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kutekeleza vyema majukumu yake ya kumshauri Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufikia malengo aliyokusudia ya kuifikisha katika hatua ya juu ya maendeleo. Vile vile, nampongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdallah, kwa kutekeleza vyema majukumu yake kama Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali. Mwenyezi Mungu awape afya njema wao na familia zao. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa dhamana ya kuiongoza Ofisi hii. Namuahidi kwamba tutatekeleza majukumu yetu kwa uweledi na ufanisi mkubwa.

4. **Mheshimiwa Spika,** shukrani na pongezi za dhati ziende kwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuteuliwa na kuapishwa kuwa Rais wa Jamuhuri ya Muunagano wa Tanzania. Tunamuombea kwa Allah amzidishie nguvu na busara za kuliongoza Taifa letu.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Kamati yetu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Welezo kwa miongozo yao wanayoendelea kuipatia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na

Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi kwa miongozo makini ya jinsi ya kuliendesha baraza letu tukufu. Pongezi hizi pia zimuendee Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa utendaji wake mzuri. Aidha, ninawapongeza watendaji wote wa Baraza lako tukufu kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia wakati wa shughuli za Baraza.

6. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi hii inashughulika na masuala mtambuka ya uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira, masuala ya Watu Wenye Ulemavu, masuala ya VVU na UKIMWI na masuala yanayohusu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Aidha, Ofisi hii inasimamia na kuratibu shughuli za Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais, pamoja na masuala ya Sera, Mipango na Tafiti za Ofisi. Ingawa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeanza kazi rasmi Disemba 2020, Taasisi zinazounda Ofisi hii zilikuwepo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na iliyokuwa Wizara ya Katiba na Sheria. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara na Taasisi zake ilijiwekea malengo yafuatayo:-

i. Kuwa na tafiti ambazo zitasaidia mipango ya maendeleo ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu ya masuala mtambuka;

ii. Usimamizi na uhifadhi madhubuti wa mazingira kwa maendeleo endelevu hapa Zanzibar;

iii. Upatikanaji na usimamizi wa haki na fursa sawa kwa Watu Wenye Ulemavu katika nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi;

iv. Udhibiti madhubuti wa uingizaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya ambao utaambatana na mikakati ya kuwapatia matibabu waathirika;

v. Kuwa na jamii isiyokuwa na maambukizo mapya ya VVU na UKIMWI;

vi. Kuwa na watumishi ambao wanatekeleza majukumu yao kwa uweledi na ufanisi.

7. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa niwasilishe utekelezaji wa mpango na bajeti kwa Idara na Taasisi zinazounda Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

***Mapato***

8. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inakusanya mapato kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira. Katika kipindi cha Julai 2020 – Machi, 2021 Ofisi hii ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 105,300,000 kutokana na vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni Ada ya Uhifadhi na Ada ya Ukaguzi wa Mazingira. Hadi kufikia Machi 2021 jumla ya shilingi 87,300,000 sawa na asilimia 83 zimekusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Matarajio yetu ni kufikia lengo la ukusanyaji kwa asilimia 100.

***Matumizi***

9. **Mheshimiwa spika,** Programu tano ambazo zilikuwa zinatekelezwa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Wizara ya Katiba na Sheria sasa zinatekelezwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Programu hizo ni

Programu ya Uendeshaji na Uratibu, Programu ya Watu Wenye Ulemavu, Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI na Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Kupitia programu hizo katika kipindi cha Julai 2020 – Machi 2021, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliidhinishiwa shilingi 5,529,267,161 katika utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi 2,305,451,507 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, na shilingi 3,223,815,654 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana hadi sasa ni shilingi 2,596,071,647. Kati ya fedha hizo shilingi 1,703,142,594 sawa na asilimia 74 kwa ajili ya mshahara na shilingi 892,929,053 sawa na asilimia 28 kwa matumizi mengineyo. (viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).

**Utekelezaji wa Malengo kwa Mwaka 2020/2021**

10. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa niwasilishe utekelezaji wa mpango na bajeti kwa taasisi zinazounda Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**B01 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

11. **Mheshimiwa Spika,** Fungu B01 linasimamia Programu tatu ambazo ni Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi na Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu.

    i. **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

12. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imeundwa na programu ndogo nne ambazo ni Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Faragha

ya Makamu wa Kwanza wa Rais; Utawala na Uendeshaji; Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti, na Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba. Kwa kipindi hiki programu hii imetekeleza yafuatayo: -

13. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Faragha imeendelea kuratibu shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais ikiwemo upatikanaji wa huduma za Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais, kufuatailia utekelezaji wa ahadi anazozitoa Mheshimiwa Makamu kwa wananchi, kutoa ufafanuzi na kutatua kero zao.

14. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, muundo wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais umeandaliwa. Muundo huu unabainisha namna ya uendeshaji na ugawaji wa majukumu ya kazi pamoja na rasilimali za Ofisi. Aidha, miundombinu ya jengo la Ofisi imeimarishwa zaidi na huduma mbali mbali za Ofisi zimeendelea kutolewa. Mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi yameendelea kuimarishwa kwa kuwapatia stahiki zao, ambapo watumishi wamepatiwa stahiki ya likizo, malipo baada ya saa za kazi na kupatiwa nyongeza za mishahara. Aidha, watumishi wawili wamelipwa stahiki za mafunzo ya muda mrefu (*angalia viambatanisho nam. 11,12&13)*.

15. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imesimamia vyema suala la utoaji wa taarifa kwa umma kwa kuandaa mikakati ya kukiwekea mazingira mazuri ya utendaji Kitengo cha Habari na Mawasiliano ya Umma na Kitengo cha Tehama kwa ununuzi wa vifaa ikiwemo camera moja ya kisasa. Aidha, kupitia vitengo hivyo, utoaji habari na mawasiliano kwa umma umeendelea kuimarika kupitia tovuti ya Ofisi *www.omkr.go.tz,* ukurasa wa facebook, youtube na instagram *ofisi*

*ya makamu wa kwanza wa rais.* Vile vile, Ofisi imeendelea kutoa taarifa mbali mbali zinazohusu ofisi kupitia mfumo wa Sema Na Rais Mwinyi (SNR) kupitia code 165 na 155. Jumla ya malalamiko 19 yameripotiwa na yanaendelea kufanyiwa kazi.

16. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanya mapitio ya awali ya sera tatu (Sera ya Watu Wenye Ulemavu 2018, Sera ya Mazingira 2013 na Sera ya VVU na UKIMWI 2012) ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziendane na mazingira na mahitaji ya sasa. Aidha, rasimu ya Sera ya Taifa ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Zanzibar inaendelea na taratibu za kukamilishwa. Kupitia Programu hii sheria tano (Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 3/2015, Sheria ya Uanzishwaji wa Tume ya UKIMWI 3/2002, Sheria ya Kusimamia na Kukinga Masuala ya UKIMWI 18/2013, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu 9/2006 na Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya 9/2009) zimefanyiwa mapitio ya awali na kubainika haja ya kufanyiwa marekebisho.

17. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeratibu shughuli zote zinazotekelezwa na Ofisi kwa upande wa Pemba ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa watumishi kwa kuwapatia stahiki zao, ambapo watumishi wamepatiwa stahiki za likizo, malipo baada ya saa za kazi na kupatiwa nyongeza za mishahara.

18. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliidhinishiwa jumla ya shilingi 3,710,672,361. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 1,686,276,507 ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara, na shilingi 2,024,395,854 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2021, jumla

ya fedha zilizopatikana kwa ajili ya mshahara ni shilingi 1,177,941,999 sawa na asilimia 70 na shilingi 663,126,722 sawa na asilimia 33 kwa matumizi mengineyo *(kiambatanisho nam. 1 kinafafanua)*.

ii. **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu**

19. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu Ofisi imeendelea kushajihisha jamii juu ya dhana ya ujumuishwaji wa Watu Wenye Ulemavu katika mipango mbali mbali ya maendeleo. Katika kipindi hiki Ofisi imetoa mafunzo kwa masheha wa Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba juu ya dhana hiyo na hivyo kushirikiana na Ofisi katika kutoa taarifa sahihi juu ya Watu Wenye Ulemavu, aina ya ulemavu, sababu za ulemavu na changamoto wanazo kabiliana nazo. Mafanikio ya kazi hii ya Usajili Shirikishi yataiwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi za Watu Wenye Ulemavu na kuweka mikakati stahiki ya kuhakikisha haki zao zinapatikana.

20. **Mheshimiwa Spika**, wanajamii kutoka maeneo mbali mbali wakiwemo wazazi na walezi wa Watoto Wenye Ulemavu, Watu Wenye Ulemavu, Maafisa Wilaya pamoja na Wajumbe wa Kamati za Shehia wameendelea kupatiwa elimu kuhusu masuala yanayohusu ulemavu. Katika kuhakisha kuwa haki na fursa za Watu Wenye Ulemavu zinazingatiwa na kutekelezwa katika taasisi za Serikali, Ofisi imesimamia utoaji wa mafunzo kwa maafisa waratibu wa Wizara katika jitihada za kuzingatia utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) nam. 9/2006 katika Wizara zao. Katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu, elimu ya lugha ya alama imeendelea kutolewa

kwa watendaji wa taasisi za Serikali, na katika kipindi hiki mafunzo hayo yametolewa kwa watendaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA).

21. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kutoa na kuratibu utoaji wa visaidizi mbali mbali Unguja na Pemba ili kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kujimudu katika shughuli zao za kila siku. Visaidizi hivyo ni pamoja na viti mwendo, pempasi na mashuka. Vile vile, ruzuku ya shilingi 7,500,000 imetolewa kwa jumuiya tatu zisizo za kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya Watu Wenye Ulemavu[1] kuziwezesha kufanya shughuli zao. Aidha, tokea kuazishwa Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu mwaka 2012, jumla ya shilingi 146,196,000 zimetolewa mkopo kwa Watu Wenye Ulemavu ili kuwawezesha kujikimu kimaisha na hadi kufikia mwezi Machi 2021, kiasi cha shilingi 20,562,500 pekee ndizo zilizorejeshwa. Ofisi kupitia Idara ya Watu Wenye Ulemavu inaendelea na jitihada za kuona namna bora ya kuweza kuusimamia Mfuko wa Maendeleo kwa Watu Wenye Ulemavu. Ufafanuzi wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Watu wenye Ulemavu unapatikana katika *kiambatanisho nam. 10*.

22. **Mheshimiwa Spika,** Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu yalifanyika tarehe 3 Disemba 2020 na ujumbe wa mwaka huo ni "*Uchumi wa Bluu Jumuishi kwa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu."* Lengo la ujumbe huu ni kujenga uelewa wa jamii juu ya mtazamo mpya wa Serikali katika kutumia fursa ya Uchumi wa Bluu. Maadhimisho haya yaliwaleta pamoja washiriki kutoka sekta za umma na sekta binafsi.

1 ZANAB, UWZ na JMZ

23. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kukuza uelewa kwa jamii juu ya masuala ya ulemavu kupitia vipindi vya redio na televisheni. Mada zilizowasilishwa ni pamoja na umuhimu wa ujumuishwaji katika masuala ya Watu Wenye Ulemavu kwenye mipango yote, miundo mbinu rafiki, umuhimu wa elimu kwa Watu Wenye Ulemavu na kuifahamu Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) nam. 9/2006.

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, programu hii iliidhinishiwa shilingi 656,198,835. Kati ya fedha hizo shilingi 268,023,634 zilipangwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 388,175,201 zilipangwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Jumla ya Fedha zilizopatikana kwa ajili ya mishahara ni shilingi 201,017,718 sawa na asilimia 75 na fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo ni 99,650,300 sawa na asilimia 26 *(kiambatanisho nam. 1 kinafafanua)*.

iii. **Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi**

25. **Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuimarisha uhifadhi na utunzaji wa mazingira pamoja na uratibu wa mabadiliko ya tabianchi Zanzibar. Programu hii inatekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) na Idara ya Mazingira.

26. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii, Ofisi imeandaa Kanuni ya Usimamizi wa Taka zinazotokana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Uandaaji wa kanuni hii unatokana na mahitaji ya sasa ambapo Zanzibar inaendelea na shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Aidha, Ofisi inaendelea na operesheni za kusimamia

upigaji marufuku mifuko ya plastiki ambapo katika kipindi hiki watu 59 wamekamatwa na kufikishwa mahakamani, ambapo washitakiwa walitozwa faini ya shilingi 4,130,000. Vile vile, jumla ya operesheni 22 za kusimamia maliasili zisizorejesheka zimefanyika Unguja na Pemba ambapo gari sita zimekamatwa na kutozwa faini ya shilingi 5,759,000. Ofisi pia imefanya ufuatiliaji katika maeneo ya mashimo ya mchanga, kifusi, kokoto, vituo vya kuchakata taka, na maeneo ya ujenzi wa kuta za kuzuia maji ya bahari ambapo miongozo ya kimazingira imetolewa kwa maeneo hayo *(kiambatanisho nam.5 kinahusika).*

27. **Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha kuwa miradi ya kiuchumi na kimaendeleo inayotekelezwa inakuwa haina uchafuzi wa mazingira, jumla ya miradi 57 imefanyiwa tathmini na kupatiwa vyeti vya kimazingira. Vile vile, Ofisi imefanya ufuatiliaji wa miradi 39 ya hoteli, uwekezaji na maendeleo katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kutokana na ufuatiliaji huo, miradi mingi imeonekana kuanza kutekeleza masharti ya mazingira. Aidha, maeneo matano ya mradi wa maji safi na salama unaosimamiwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) yamefanyiwa ufuatiliaji wa kimazingira na kutolewa muongozo wa usimamizi wake. Vile Vile, jumla ya taarifa 21 zinazohusiana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira zimepokelewa na zimefanyiwa kazi *(angalia viambatanisho nam. 6,7&8).*

28. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kuishirikisha jamii juu ya masuala ya uhifadhi wa mazingira, Ofisi imefanya mikutano na wananchi katika Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi ‘B’. Aidha, ili kukuza uelewa na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira Ofisi imetayarisha na kurusha vipindi vya redio na televisheni na kushiriki

katika Tamasha la Saba la Biashara *(angalia kiambatanisho nam 9).*

29. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa jamii, Ofisi inatekeleza mradi wa Kukuza Uwezo wa Kitaifa wa kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi na Maisha ya Jamii kupitia Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Kifaa cha hali ya hewa '*Automatic Weather Station'* kimenunuliwa na kiko katika taratibu za kufungwa katika eneo la Skuli ya Pindua, Mkoani Pemba.

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, katika kutekeleza programu hii, jumla ya shilingi 569,028,746 ziliidhinishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa kazi za kawaida ambapo shilingi 375,831,631 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 193,197,115 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2021, shilingi 322,295,605 sawa na asilimia 86 zilipatikana kwa ajili ya mishahara na shilingi 55,735,000 sawa na asilimia 29 ni kwa matumizi mengineyo. Aidha, Idara ya Mazingira iliidhinishiwa shilingi 425,116,120 kwa kazi za kawaida ambapo shilingi 272,592,082 kwa ajili ya mishahara na shilingi 152,524,038 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2021, Idara iliingiziwa shilingi 205,187,090 sawa na asilimia 75 kwa ajili ya mishahara na shilingi 52,210,291 sawa na asilimia 34 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Programu hii iliidhinishiwa kutumia shilingi 1,265,712,000 kwa kazi za maendeleo ambapo shilingi 300,000,000 ni mchango wa Serikali na shilingi 965,712,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (UNDP 289,800,000 na AfDB 675,912,000). Hadi kufikia Machi, 2021, shilingi 152,444,000 zilipatikana

kwa kazi za maendeleo, sawa na asilimia 12, (ambapo shilingi 6,854,000 kutoka AfDB na shilingi 145,590,000 ni kutoka UNDP). Hakuna fedha iliyopatikana kama mchango wa Serikali *(angalia viambatanisho nam. 1&4).*

**C04 – Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya – Programu ya Udhibiti wa Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya**

31. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, yenye lengo la udhibiti wa usafirishaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini ili kuwa na jamii ambayo imeepukana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2020, kesi zilizopelekwa mahakamani ni 214 ambapo zilizopata hatia ni 28, zilizoachiwa huru 5, zilizofungwa Polisi 18, zilizoko kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ni 13, zenye hati ya mashtaka 36 na zilizo chini ya upelelezi ni 140. Katika kipindi hiki, jumla ya wageni 7 walikamatwa na kilogramu 22.7 ambapo kesi nne zinaendelea mahakamani, kesi moja imehukumiwa kifungo miaka 14 jela, moja imefutwa mahakamani, moja imehukumiwa kifungo cha miaka 25 jela na faini ya shilingi 20,000,000.

32. **Mheshimiwa Spika,** kesi nyingi zinaonekana kubakia mahakamani na nyengine chini ya upelelezi wa Polisi kwa sababu mbali mbali zikiwemo, mashahidi kutokufika mahakamani na hivyo kesi kusogezwa mbele ama kuwepo kwa baadhi ya watendaji wa kimahakama wasiokuwa waaminifu ambao huziahirisha kesi au kutoa dhamana kinyume na utaratibu. Vile vile, kesi zimebakia katika upelelezi wa Polisi muda mrefu kutokana na kuchelewa kukamilika kwa upelelezi kunakosababishwa na Maofisa kutokuwa na taaluma ya kutosha ya upelelezi. Pia, kesi

zinafungwa katika Vituo vya Polisi kutokana na aidha, kutokukamilika kwa ushahidi au kesi kukaa muda mrefu bila kupelekwa mahakamani na wakati mwingine baadhi ya kesi watuhumiwa wake wameachiliwa kwa sababu ya mahakama kutoridhika na ushahidi uliotolewa wa kumtia hatiani mtuhumiwa.

33. **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi wa vielelezo umefanyika mwaka 2020 ambapo kiwango cha dawa kinachokisiwa kuwepo ni kilogramu 124.024 kinasubiri kuteketezwa ingawaje kiwango halisi cha dawa hizo kitathibitishwa siku ya uteketezaji. Katika kuharakisha uendeshaji wa kesi za dawa za kulevya; rasimu ya muongozo wa mfumo wa uendeshaji wa pamoja wa kushughulikia kadhia ya dawa za kulevya ambao utahusisha Taasisi zote za usimamizi wa sheria imeandaliwa na kukamilika ikisubiri hatua za uthibitishwaji wake. Aidha, katika kuhakikisha tunaikinga jamii na athari ya dawa za kulevya, wakiwemo watoto, programu ya kinga ya msingi (primary prevention) imeandaliwa na kutekelezwa kwa kutoa elimu kwa watoto wa skuli za maandalizi ili kuwajengea uwezo wa kujikinga na kukabiliana na vichocheo vitakavyopelekea kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Jumla ya wanafunzi 70 wa skuli za Maandalizi za Serikali walipatiwa taaluma hiyo.

34. **Mheshimiwa Spika**, Tume kupitia programu hii imezipatia nyumba sita za Upataji Nafuu (Sober Houses) Ruzuku ya shilingi 1,500,000 kwa Unguja na Pemba kila moja kwa lengo la kuchangia uendeshaji wa nyumba hizo. Aidha, katika kuhakikisha kuna ushirikiano wa pamoja, mikutano na Kamati za Ulinzi na Usalama za Shehia zilizoathiriwa na uuzaji na matumizi ya dawa za kulevya Unguja na Pemba imefanyika na kuwapatia washiriki elimu, mwamko na

mbinu mbadala za kupambana na janga la dawa za kulevya katika maeneo yao. Vile vile, mikutano ya Tiba ya Kifamilia (Family Therapy) imefanyika iliyozishirikisha familia 86 zenye watu wanaotumia dawa za kulevya na waliopata nafuu Unguja na Pemba ili kuwaweka karibu na familia zao wale walioacha matumizi ya dawa za kulevya na kuondosha unyanyapaa. Aidha, Tume imeendelea kushirikiana na taasisi za Kikanda na Kimataifa[2] za kupambana na dawa za kulevya ili kuweza kuimarisha mtandao wa mapambano hayo. Kwa kushirikiana na Taasisi hizo Tume imeratibu mafunzo Maalum ya Ulinzi na Usalama wa Bandari (Port Security) kwa watendaji wa taasisi za Serikali[3].

35. **Mheshimiwa Spika,** Tume imetoa mafunzo kwa wasimamizi wa sheria ambao ni Waheshimiwa Majaji, Mahakimu, Waendesha Mashtaka na Wakuu wa Upelelezi kutoka Jeshi la Polisi kuhusiana na uendeshaji wa kesi za dawa za kulevya, utunzaji wa vielelezo, Sheria za maadili pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Vile vile, Tume imeendelea kutoa elimu kwa jamii wakiwemo wanafunzi na walimu wa skuli za msingi, sekondari na vyuo vikuu Unguja na Pemba na vile vile, elimu imetolewa kupitia vyombo vya habari. Aidha, elimu ilitolewa kwa jamii kupitia maonesho ya Tamasha la Saba la Biashara katika maadhimisho ya miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

36. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Uendeshaji na Utawala Tume imeendelea kuweka mazingira mazuri ya

---

2 UNODC, Drug Enforcement Administration, US Department of Defence- Bureau of International Narcotics & Law Enforcement Affairs na British Borders.

3 Tume, Jeshi la Polisi, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), Idara ya Usalama wa Taifa, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Shirika la Bandari, Bodi ya Mapato Tanzania na Mamlaka ya Usafiri Baharini.

ofisi kwa upatikanaji wa huduma za ofisi, mafunzo na stahiki nyengine za wafanyakazi.

**37. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai 2020 – Machi, 2021, programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 848,452,800. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 243,075,000 zilipangwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 605,377,800 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana kwa ajili ya mshahara ni shilingi 297,006,490 sawa na asilimia 122 na shilingi 166,874,831 sawa na asilimia 28 kwa matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizopangwa ni 1,900,000,000 lakini hakuna fedha iliyopatikana *(viambatanisho 1&4 vinahusika)*.

**CO5 - Tume ya UKIMWI - Programu ya Kuratibu Mwitiko wa Taifa wa UKIMWI**

**38. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya UKIMWI ya Zanzibar (ZAC) na lengo lake ni kuhakikisha kwamba maambukizo ya Virusi vya UKIMWI yanapungua kwa kuratibu shughuli za kupunguza maambukizo na kuelimisha jamii kuhusu kujikinga na maambukizo ya Virusi vya UKIMWI na athari za unyanyapaa kwa walioathirika. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya watu 8,147 wamegundulika kuwa na Virusi vya UKIMWI, kati ya hao wanawake ni 5,621 na wanaume ni 2,526 Unguja na Pemba.

**39. Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma jumuishi kwa kliniki za tiba na vituo rafiki kwa vijana Unguja na Pemba. Katika vituo hivi huduma zinazotolewa ni pamoja na zile za UKIMWI na uzazi wa mpango na uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi kwa watu wanaoishi na VVU ambapo hadi kufikia Machi 2021, wanawake 1,075 wanaoishi na VVU wamepatiwa

huduma za uzazi wa mpango kupitia kliniki za tiba. Aidha, wanawake 1,138 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi. Kati yao watu 16 waligundulika na dalili za mwanzo za saratani na hivyo kupewa rufaa kwa ajili ya matibabu husika. Vile vile, vijana 4,918 walipata huduma katika vituo rafiki ikiwemo upimaji wa VVU ambapo vijana 4,534 walipima na 197 waligundulika kuwa na VVU Unguja na Pemba.

40. **Mheshimiwa Mwenyekeiti,** Ofisi kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia[4] imetekeleza Programu ya kuyanusuru makundi maalum ya wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao, wanawake wanaojiuza na watu wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga sindano. Takwimu zinaonesha kwamba hadi kufikia Machi 2021 watu 5,974 wa makundi maalumu walifikiwa na huduma za VVU. Kati ya hao 4,128 walipima na 40 waligunduliwa kuwa na maambukizo. Viwango vya maambukizo ya VVU katika makundi haya viko juu ambapo ripoti za utafiti zinaonesha kwamba asilimia 5.0 ya wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao (sawa na watu 150) wanaishi na VVU, asilimia 5.1 ya wanaojidunga sindano (ikiwa ni sawa na watu 112) na asilimia 12.1 ya wanawake wanaojiuza (ikiwa ni sawa na watu 587).

41. **Mheshimiwa Spika,** kundi la vijana la miaka 15-24 ni miongoni mwa makundi yanayoongoza kupata maambukizo mapya ya VVU. Jitihada maalum zilifanywa kuwafikia vijana na kuwapa fursa ya kupima afya zao kupitia kampeni maalum iliyojulikana kwa jina la "Kijana Kataa UKIMWI". Jumla ya vijana 3,098 walipima VVU (1,577 wanaume na 1,521 wanawake) ambapo vijana 16 waligundulika na VVU

4 ZAPHA+, ZAYEDESA, UMATI, JUKAMKUM, ZANGOC na AYAHIZA

(wanawake 11 na wanaume 5) nao wamegundulika kuwa na VVU.

42. **Mheshimiwa Spika**, njia ya kujamiiana inachukua zaidi ya asilimia 70 ya maambukizo yote ya VVU yanayotokezea. Ili kudhibiti maambukizo yanayotokana na kujamiiana kusiko salama, elimu kwa jamii imetolewa kupitia njia mbali mbali ikiwemo maonesho na matamasha, bonanza la michezo kwa vijana, burudani, shindano la mpira wa miguu, ugawaji wa machapisho na vipeperushi. Ofisi pia imeongeza upatikanaji wa taarifa na elimu kuhusu VVU na UKIMWI kupitia tovuti na mitandao ya kijamii (instagram[5] na facebook[6]) pamoja na vipindi vya redio vikiwemo vipindi maalum vinavyowahusu vijana.

43. **Mheshimiwa Spika**, Maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani yalifanyika tarehe 1 Disemba 2020, yakiwa na ujumbe, "*Tushikamane Tuwajibike Kumaliza UKIMWI'*. Lengo la maadhimisho ni kujadili kwa pamoja mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika kutekeleza shughuli za kupambana na maambukizo ya UKIMWI na unyanyapaa.

44. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeshughulikia na kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi kwa kusimamia maslahi na stahiki za wafanyakazi, upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi na utoaji wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

45. **Mheshimiwa Spika** kwa mwaka wa fedha wa 2020/21, Tume ya UKIMWI ilitengewa jumla ya shilingi 970,142,000 ambapo kati ya hizo 376,100,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi milioni 594,042,000 ni kwa ajili ya matumizi

---

5 Zanzibaraidscommission

6 TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

mengineyo. Hadi kufikia Machi 2021, fedha zilizoingizwa kwa mishahara ni 228,194,105 sawa na asilimia 61 na shilingi 62,927,500 sawa na asilimia 11 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Tume imepokea shilingi 334,821,849 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo[7] *(viambatanisho 1&4 vinahusika).*

## C. MUELEKEO WA PROGRAMU ZA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**46.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020/2021 sasa naomba kutoa maelezo ya muelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**47.** Dira ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Taasisi zake ni '*kuwa sehemu ya ujenzi wa uchumi imara na salama, shirikishi, endelevu na himilivu'*. Ofisi itashiriki kwenye kujenga uchumi imara kwa kuimarisha mifumo kuwa bora zaidi, madhubuti na endelevu ya kusimamia masuala mtambuka ya Watu Wenye Ulemavu, Mazingira, VVU na UKIMWI pamoja na udhibiti wa Dawa za Kulevya. Dira hii inakwenda sambamba na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030, Ilani ya Chama cha Mapindunzi 2020 -2025, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi na Maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa kwa Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** muono wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni kwenda sambamba na sera na mikakati

---

7 UNAIDS, UNFPA, GF, UNICEF, CDC na PEPFAR

iliyowekwa na Serikali ya kufikia malengo ya uchumi na kuhakikisha kuwa wananchi wa makundi yote wanawezeshwa na kuwa sehemu ya ujenzi wa uchumi huo. Kwa kutambua kuwa asilimia kubwa ya wajenzi wa uchumi wa Zanzibar ni vijana ambao wamo kwenye hatari ya kuathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya, Ofisi itaendelea kuwasaidia kutokujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya na kuwakinga wasiambukizwe Virusi vya UKIMWI. Aidha, Ofisi ina dhamira ya kusaidia kujenga uchumi shirikishi na endelevu utakaohakikisha ujumuishi wa Watu Wenye Ulemavu.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia Dira tuliyojiwekea, tutaimarisha uwajibikaji kwa watendaji, kufanya mapitio ya miundo ya baadhi ya taasisi, kuwashirikisha na kuwaweka wadau kwa karibu zaidi pamoja na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ikiwemo utoaji wa taaluma na ushajihishaji wa wananchi kwa kutumia mbinu za kisasa zaidi. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeweka vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuwa na tafiti ambazo zitasaidia mipango ya maendeleo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya masuala mtambuka;

ii. Usimamizi na uhifadhi madhubuti wa mazingira kwa maendeleo endelevu hapa Zanzibar;

iii. Upatikanaji na usimamizi wa haki na fursa sawa kwa Watu Wenye Ulemavu katika nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi;

iv. Udhibiti madhubuti wa uingizaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya ambao utaambatana na mikakati ya kuwapatia matibabu waathirika;

v. Kuimarisha na kusimamia mipango ya kudhibiti maambukizo mapya ya VVU.

vi. Kuendelea kuimarisha mazingira ya utendaji kazi pamoja na kutoa stahiki za watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ueledi na ufanisi;

vii. Kufanya uchambuzi (analysis) wa kina wa nyenzo mbali mbali zinazoongoza utendaji katika Sekta Mtambuka zinazosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili kuweza kuziratibu utekelezaji wake.

**B01 – Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

**50. Mheshimiwa Spika,** Fungu B01 linahusika na kuratibu kwa ukaribu zaidi masuala yote yanayohusu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais yakiwemo masuala ya Watu Wenye Ulemavu, udhibiti wa dawa za kulevya, usimamizi wa mazingira na masuala ya UKIMWI ili kuhakikisha kuwa jamii inanufaika na huduma zote zinazotolewa na Serikali kwa masuala hayo. Masuala ya mazingira yatapewa umuhimu wa hali ya juu katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inafanikiwa kwa kiasi kikubwa kukabiliana na changamoto zote za mazingira zitakazojitokeza. Vile vile, uratibu juu ya masuala ya kudhibiti dawa za kulevya utatekelezwa kwa kiasi kikubwa kwa kuweka mikakati madhubuti zaidi ya kiutendaji. Sera, sheria, kanuni na miongozo yote itapewa umuhimu wa kipekee kwa kuzifanyia mapitio, kuzirekebisha au kutungwa upya pale itakapohitajika ili kufanikisha ufikishaji wa huduma kwa jamii. Aidha, ushirikiano na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyingine utaendelea kuimarishwa katika kuratibu masuala ya kikanda

na kimataifa yanayohusu Mazingira, UKIMWI, Dawa za Kulevya na Watu Wenye Ulemavu. Fungu hili linasimamia programu kuu nne zifuatazo: -

i. **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

51. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii masuala yote yanayohusu mipango, usimamizi wa rasilimali watu, uratibu wa shughuli za Ofisi Kuu Pemba na uratibu wa shughuli za Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais yanasimamiwa.

52. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, mazingira ya utendaji kazi yataimarishwa zaidi ikiwemo stahiki za likizo, stahiki za malipo baada ya saa za kazi na stahiki nyengine. Ofisi pia itaendelea kuimarisha na kuwajengea uwezo watendaji kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

53. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti, Ofisi itaratibu na kufanya tafiti tatu zinazohusiana na masuala ya Watu Wenye Ulemavu na UKIMWI pamoja na kuzipitia sera na sheria zinazosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili ziendane na wakati wa sasa. Vile vile, kupitia programu hii ofisi imepanga kuwa na mfumo imara na madhubuti wa kuhifadhi takwimu za shughuli zote zinazotekelezwa pamoja na kuwa na mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ambao utatumika kufuatilia shughuli na miradi yote inayotekelezwa.

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba imejipangia kuratibu na kutekeleza mambo yote

yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ikiwemo suala la usimamizi wa Mazingira, masuala ya Watu Wenye Ulemavu, mapambano dhidi ya UKIMWI na udhibiti wadawa za kulevya kwa upande wa Pemba. Vile vile, Ofisi itaendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa ununuzi wa vifaa na samani na suala zima la usafiri. Aidha, watumishi watajengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu pamoja na kupatiwa stahiki zote.

### ii. Programu ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais

55. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais itahakikisha huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais zinapatikana. Aidha, itaendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi anazozitoa Mheshimiwa Makamu kwa wananchi pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya utatuzi wa kero za wananchi zinazowasilishwa kwa Mheshimiwa Makamu.

### iii. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

56. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii Ofisi itaendelea kufanya usajili wa Watu Wenye Ulemavu Katika Mfumo wa Jumuishi ili kurahisisha upatikanaji wa elimu na uwezeshwaji kiuchumi ikiwemo kuwaunganisha na taasisi mbali mbali za kifedha kwa kuwapatia mitaji na kukuza fursa za ajira. Hadi kufikia Machi 2021, watu 8,380 wameshasajiliwa katika mfumo wa kuhifadhia taarifa za Watu Wenye Ulemavu (Jumuishi Data Base). Katika kipindi hiki Ofisi imepanga kusajili Watu Wenye Ulemavu

2,500. Ofisi pia imeweka shabaha ya kupunguza idadi ya Watu Wenye Ulemavu unaotokana na ajali za barabarani na magonjwa yasiyoambukiza. Mikutano ya pamoja na mamlaka mbali mbali zinazohusiana na sekta ya usafirishaji na afya itafanyika ili kupunguza uwezekano wa kupata ulemavu. Kampeni mbali mbali za kuhamasisha mazoezi ya viungo na ulaji sahihi wa chakula yatapewa kipaumbele ili kuimarisha afya na kupunguza uwezekano wa magonjwa ya kisukari na shinikizo la damu.Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi nyengine Zisizo za Kiserikali itaendelea kuwapatia visaidizi Watu Wenye Ulemavu kulingana na ulemavu wao. Ofisi itaendelea kuzijengea uwezo taasisi za serikali hususan zile zinazotoa huduma kwa kuwapatia taaluma ya lugha ya alama wakiwemo watendaji wa Idara ya Watu Wenye Ulemavu Pemba. Vile vile, itafanya uhamasishaji kwa jamii kupitia vipindi vya redio na televisheni ili Watu Wenye Ulemavu wapate haki na fursa.

**iv. Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi**

57. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa kwa pamoja na Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira. Lengo la programu hii ni kuhakikisha usimamizi endelevu wa mazingira. Shabaha zilizowekwa kufikia lengo hili ni kusimamia ripoti 70 za tathmini za kimazingira na kufuatilia miradi 192, maeneo ya mazingira 192, operesheni za mifuko ya plastiki ni 120, na maliasili zisizorejesheka 168.

58. **Mheshimiwa Spika,** kama tunavyotambua kuwa Zanzibar, kama zilivyo nchi nyengine duniani, ipo katika hatari za kimazingira na inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hivyo Ofisi itaendelea na jitihada za kutoa

miongozo ya jinsi ya kuhimili athari ya mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Unguja na Pemba ikiwemo Msuka, Tovuni na Bumbwini Mafufuni pamoja na kuwapatia mbinu mbadala za kujikimu kimaisha wananchi walioko katika maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi hususan katika sekta ya kilimo na uvuvi. Aidha, Ofisi itaendelea kufanya operesheni za upigaji marufuku mifuko ya plastiki na kusimamia maliasili zisizorejesheka.

59. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi itahakikisha kuwa tathmini za athari za kimazingira na kijamii, zinafanywa kwa miradi yote ya kimaendeleo na kiuchumi, ili kuifanya miradi hiyo kuwa endelevu. Aidha, ufatiliaji wa kimazingira kwa maeneo ya miradi ya kiuchumi na kimaendeleo Unguja na Pemba itaendelea ili kuhakikisha tunapunguza uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa kutoa miongozo mbali mbali.

60. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi itaendelea kulipa kipaumbele suala kukuza ushiriki wa jamii katika utunzaji na usimamizi bora wa mazingira kwa kutoa elimu ya vitendo kwa jamii kwa kutumia njia mbali mbali pamoja na kufanyakazi na Asasi za kiraia zinazoshughulikia mazingira Unguja na Pemba.

61. **Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Fungu B01 liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 7,661,159,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,840,300,000 (76%) zimetengwa kwa matumizi ya kawaida zikiwemo shilingi 2,293,200,000 za mishahara na shilingi 3,547,100,000 za matumizi mengineyo; na shilingi 1,820,859,000 (24%) zimetengwa kwa shughuli za maendeleo zinazojumuisha shilingi 300,000,000 kutoka Serikalini na shilingi 1,520,859,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (*kiambatanisho nam. 2).*

## C04 – Tume ya Kitaifa Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya – Programu ya Udhibiti wa Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya

62. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imelenga kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kudhibiti usafirishaji usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya na kuweka mikakati imara ya upataji nafuu kwa waathirika. Ofisi itaendelea kuratibu na kuendeleza mapambano juu ya usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya na kuanza kazi kwa mfumo wa kuharakisha ufatiliaji wa kesi za dawa za kulevya kupitia utoaji wa huduma za pamoja za uendeshaji wa kesi za dawa za kulevya. Mwelekeo wa mfumo huu ni kuwa na kituo cha pamoja cha kushughulikia mwenendo wa kesi za dawa za kulevya (one stop centre). Pia, ofisi itaratibu upatikanaji wa vifaa vya uchunguzi (body screens) vya kuwatambua na kuwakamata wanaoingiza dawa za kulevya.

63. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi itakifungua na kuendesha Kituo cha Upataji Nafuu na Marekebisho ya Tabia Kidimni; itaendeleza ujenzi na itaendesha Programu za Upataji Nafuu; kuendelea kuzisaidia nyumba za upataji nafuu na kurekebisha tabia (sober houses) na utoaji wa elimu kupitia vyombo vya habari juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya. Hata hivyo mapambano ya vita dhidi ya dawa za kulevya yanahitaji pia nguvu kubwa kutoka kwa jamii .Katika kuhakikisha tunapunguza na kuondoa kabisa usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya, Ofisi itafanya zoezi la kupitia vielelezo vya dawa za kulevya zilizokamatwa na kuhifadhiwa mahakamani na vituo vya Polisi pamoja na kusimamia zoezi la kuteketeza dawa hizo.

64. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi itaendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na utendaji kazi kwa wafanyakazi kwa upatikanaji wa vyombo vya usafiri na samani na kuendelea kulipa stahiki za wafanyakazi pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

65. **Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Fungu C04 liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 3,174,100,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,274,100,000 kwa matumizi ya kawaida ambapo shilingi 399,900,000 ni za mishahara na shilingi 874,200,000 ni matumizi mengineyo. Shilingi 1,900,000,000 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo kutoka Serikalini (*kiambatanisho nam. 2)*.

## C05 – Tume ya UKIMWI - Programu ya Kuratibu Mwitiko wa Taifa wa UKIMWI

66. **Mheshimiwa Spika,** shabaha ya programu hii ni kupunguza maambukizo mapya kutoka watu 227 (2020/2021) mpaka 170 (2021/2022). Ofisi imejipanga kuongeza kasi ya uhamasishaji kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya tabia yatakayopelekea kudhibiti maambukizo mapya ya VVU katika jamii na makundi maalum, kuishajiisha jamii na sekta zote zikiwemo sekta binafsi kushiriki katika mapambano dhidi ya UKIMWI katika sehemu zao na kuimarisha uwezo wao kwa kuweka miongozo na kuwapatia elimu na maarifa ya kutekeleza mipango yao kwa ufanisi. Aidha, Ofisi imepanga kuimarisha mazingira ya kutendea kazi ikiwemo kutafuta rasilimali, kuongeza utaalamu kwa wafanyakazi na upatikanaji wa vitendea kazi.

67. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi imepanga kufanya utafiti juu ya Athari za Ukuaji wa Utalii kwa Maambukizo ya VVU

Zanzibar na kuanza maandalizi ya utafiti wa Kiwango cha Maambukizo ya VVU katika jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na asasi za kiraia zinazotekeleza programu za uhamasishaji za ushauri nasaha, elimu, huduma na rufaa kwa makundi maalum na watoto wanaoishi na VVU. Aidha, ofisi imepanga kutayarisha Mkakati wa IV wa Kupambana na UKIMWI; kuifanyia mapitio Sera ya UKIMWI na Sheria nam. 18/2014 na kanuni zake. Jitihada za kuwajengea uwezo Taasisi za Serikali na binafsi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, NGOs na jamii ili ziweze kuchangia kudhibiti maambukizo mapya ya VVU zitaendelezwa. Aidha, Tume itaendelea kuhamasisha wadau wa sekta ya ujenzi, viwanda na uvuvi kuzingatia masuala ya UKIMWI katika maeneo yao; kuandaa maandiko ya miradi mbali mbali; na kuendeleza jitihada za kuandaa Mfuko wa UKIMWI ili kupata rasilimali kwa ajili ya Muitiko wa Kitaifa wa VVU na UKIMWI.

68. **Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Fungu C05 liweze kutekeleza majukumu yake, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 1,345,800,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,194,843,000 kwa matumizi ya kawaida ambapo shilingi 452,900,000 ni za mishahara na shilingi 741,943,000 na matumizi mengineyo. Shilingi 150,957,000 zimetengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (*kiambatanisho nam. 2)*.

## D. SHUKURANI

69. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo hayo, nachukua fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako Tukufu. Kwa namna ya kipekee kabisa ninamshukuru Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa

utendaji wake makini. Aidha, ninawashukuru watumishi na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Bila ya wao hata hii hotuba yetu isingewezekana kukamilishwa. Aidha, ninamshukuru aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Bi Kheriyangu Khamis Mgeni na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya UKIMWI, Dkt. Ahmed M. Khatib.

70. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuzishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), TASAF, Tume ya Haki za Binaadam, pamoja na nchi za Norway na Uingereza. Nawashukuru Washirika wa Maendeleo waliofanya kazi pamoja nasi ambao ni UNDP, UNEP, Global Environment Facility (GEF), Green Climate Fund (GCF), Adaptation Fund, UNODC, UK- Border Force, UNFPA, UNICEF, Zanzibar Early Childhood Program, Zanzibar Milele Foundation, Global Fund, PEPFAR, na UNAIDS. Vile vile, nazishukuru taasisi zote zisizo za kiserikali zilizofanyakazi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

71. **Mheshimiwa Spika,** navishukuru vyombo vya habari kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa elimu na kutangaza matukio mbali mbali yanayohusu shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninawashukuru wahusika wote walioshirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

## E. **HITIMISHO**

**72. Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kuelekea kuimarisha zaidi ustawi wa wananchi wetu. Ninamuomba Mwenyeezi Mungu azidi kumpa nguvu na busara katika kutekeleza majukumu yake ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

**73. Mheshimiwa Spika,** naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais shilingi **12,181,059,000** ili kutekeleza kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya fedha hizo, shilingi **8,309,243,000** ni kwa matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi **3,146,000,000** matumizi mengineyo ni shilingi **5,163,243,000;** na Shilingi **3,871,815,600** ni kwa matumizi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao.

| TAASISI/IDARA | KIASI (Shilingi) |
|---|---|
| Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,612,729,000 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 345,376,000 |
| Ofisi ya Faragha | 702,740,000 |
| Ofisi Kuu Pemba | 1,038,497,000 |
| Idara ya watu Wenye Ulemavu | 913,150,000 |
| Idara ya Mazingira | 2,370,887,000 |
| Mamlaka ya Mazingira | 677,780,000 |
| Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa dawa za Kulevya | 3,174,100,000 |
| Tume ya UKIMWI | 1,345,800,000 |
| **JUMLA KUU** | **12,181,059,000** |

74. **Mheshimiwa Spika,** aidha naliomba Baraza lako tukufu liikubalie Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ichangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya shilingi **173,400,000** zitakazokusanywa kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira *(viambatanisho 2&3 vinahusika)*.

75. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Kiambatanisho nam. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha Julai 2020 - Machi 2021 (000)**

| Fungu/Idara | Jumla ya Matumizi ya Kawaida | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Jumla ya Fedha Zilizopatikana | % | Mishahara Iliyopatikana | % | Fedha za Matumizi Mengineyo Zilizopatikana | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Progamu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais** | | | | | | | | | |
| Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,250,327 | 476,634 | 773,693 | 500,415 | **40** | 238,790 | **50** | 261,626 | **34** |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 324,079 | 110,190 | 213,890 | 143,898 | **44** | 66,127 | | 77,771 | **36** |
| Ofisi Kuu Pemba | 485,922 | 183,006 | 302,917 | 260,660 | **54** | 144,525 | **79** | 116,135 | **38** |
| **Jumla ya Programu ya Uendeshaji na Uratibu OMKR** | **2,060,328** | **769,830** | **1,290,500** | **904,973** | | **449,442** | | **455,532** | |

| Fungu/Idara | Jumla ya Matumizi ya Kawaida | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Jumla ya Fedha Zilizopatikana | % | Mishahara Iliyopatikana | % | Fedha za Matumizi Mengineyo Zilizopatikana | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu kuu ya Watu Wenye Ulemavu** | | | | | | | | | |
| **Idara ya Watu Wenye Ulemavu** | **656,199** | **268,024** | **388,175** | **300,668** | **46** | **201,018** | **75** | **99,650** | **26** |
| **Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira** | | | | | | | | | |
| Mamlaka ya Usimazi wa Mazingira | 569,029 | 375,832 | 193,197 | 378,031 | **66** | 322,296 | **86** | 55,735 | **29** |
| Idara ya Mazingira | 425,116 | 272,592 | 152,524 | 257,397 | **61** | 205,187 | **75** | 52,210 | **34** |
| **Jumla ya Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira** | **994,145** | **648,424** | **345,721** | **635,428** | | **527,483** | | **107,945** | |

**Programu kuu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI**

| Fungu/Idara | Jumla ya Matumizi ya Kawaida | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Jumla ya Fedha Zilizopatikana | % | Mishahara Iliyopatikana | % | Fedha za Matumizi Mengineyo Zilizopatikana | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tume ya UKIMWI | 970,142 | 376,100 | 594,042 | 291,122 | 30 | 228,194 | 61 | 62,928 | 11 |
| Tume ya Kitaifa ya KUD | 848,453 | 243,075 | 605,377,800 | 463,881 | 55 | 297,006 | 122 | 166,875 | 28 |
| JUMLA KUU | 5,529,267 | 2,305,452 | 3,223,816 | 2,596,072 | 47 | 1,703,143 | 74 | 892,929 | 28 |
| JUMLA B01 | 3,710,672 | 1,686,277 | 2,024,396 | 1,841,069 | 50 | 1,177,942 | 70 | 663,127 | 33 |
| JUMLA CO4 - C05 | 1,818,595 | 619,175 | 1,199,420 | 755,003 | 42 | 525,201 | 85 | 229,802 | 19 |

## Kiambatanisho nam. 2: Muelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 (000)

| Programu | Kazi za Kawaida | | | | Kazi Za Maendeleo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Mishahara na Stahiki | Matumizi Mengineyo | SMZ | Washirika wa Maendeleo | Jumla Maendeleo | Jumla Kuu |
| **Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira** | | | | | | | |
| Idara ya Mazingira | 550,028 | 288,817 | 261,211 | 300,000 | 1,520,859 | 1,820,859 | 2,370,887 |
| Mamalaka ya Usimamizi wa Mazingira | 677,780 | 425,980 | 251,800 | - | - | - | 677,780 |
| **Jumla ya Programu Kuu ya Usimamizi wa Mazingira** | **1,227,808** | **714,797** | **513,011** | **300,000** | **1,520,859** | **1,820,859** | **3,048,667** |
| **Programu kuu ya Watu Wenye Ulemavu** | | | | | | | |
| **Idara ya Watu Wenye Ulemavu** | **913,150** | **325,150** | **588,000** | **-** | **-** | **-** | **913,150** |
| **Progamu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais** | | | | | | | |
| Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,612,729 | 688,110 | 924,619 | - | - | - | 1,612,729 |

| Programu | Kazi za Kawaida | | | | Kazi Za Maendeleo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Mishahara na Stahiki | Matumizi Mengineyo | SMZ | Washirika wa Maendeleo | Jumla Maendeleo | Jumla Kuu |
| Idara ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | 345,376 | 132,376 | 213,000 | - | - | - | 345,376 |
| Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba | 1,038,497 | 432,767 | 605,730 | - | - | - | 1,038,497 |
| **Jumla ya Progamu ya Uendeshaji na Uratibu wa OMKR** | **2,996,602** | **1,253,253** | **1,743,349** | **-** | **-** | **-** | **2,996,602** |
| **Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais** | | | | | | | |
| **Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais** | **702,740** | **-** | **702,740** | **-** | **-** | **-** | **702,740** |
| **Progrmu Kuu ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya** | | | | | | | |
| **Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya** | **1,274,100** | **399,900** | **874,200** | **1,900,000** | **-** | **1,900,000** | **3,174,100** |
| **Progrmu kuu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI** | | | | | | | |
| **Tume ya UKIMWI** | **1,194,843** | **452,900** | **741,943** | **-** | **150,957** | **150,957** | **1,345,800** |
| **JUMLA KUU** | **8,309,243** | **3,146,000** | **5,163,243** | **2,200,000** | **1,671,815.6** | **3,871,815.6** | **12,181,059** |

**Kiambatanisho nam. 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai-Machi 2020/2021 na Makadirio ya 2021/2022**

| Kifungu | Idara /Taasisi | Makadirio 2020/2021 | Makusanyo Halisi | % | Makadirio 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| B01 | **B01 Mamlaka ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira** | 105,300,000 | 87,300,000 | 83 | 173,400,000 |

**Kiambatanisho nam. 4: Miradi ya Maendeleo Inayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

| Sekta | Jina la Mradi | Thamani | Chanzo | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| Mazingira | 1. Kujenga Uwezo wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabia Nchi – Zanzibar "*Enhancing National Capacity for Mainstreaming Climate Resilience in Zanzibar.*" | 361,515 (US $) | AfDB | Idara ya Mazingira |
| Mazingira | 2. Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa | 7,571,233 (US $) | UNEP | Idara ya Mazingira |

| Sekta | Jina la Mradi | Thamani | Chanzo | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| | Kutumia Mfumo Ikoloji Vijijini - Tanzania 'Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience' – Tanzania | | | |
| Mazingira | 3. Kuimarisha Uhimili Wa Mabadiliko Ya Tabianchi (*Enhancing Climate Change Resilience in Zanzibar)* | 1,000,000 (US $) | UNDP | Idara ya Mazingira |
| Mazingira | 4. Kuimarisha Uhimili Wa Mabadiliko Ya | 1,000,000 (US $) | Adaptation | Idara ya |

| Sekta | Jina la Mradi | Thamani | Chanzo | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| | Tabianchi Kwa Jamii za Pwani ya Zanzibar *"Enhancing Climate Change Resilience of Coastal Communities of Zanzibar* | | Fund | Mazingira |
| Mazingira | 5. Ukuzaji Wigo na Uongezaji wa Kiwango cha Ufanisi cha Mtambo wa Kusafisha Maji | 298,500 (US $) | UNEP | Idara ya Mazingira |

| Sekta | Jina la Mradi | Thamani | Chanzo | Mhusika |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | Taka wa Msingini, Chake Chake, Pemba "*Upscaling and Amplification of the Msingini Waste Water Treatment Facility*" | | | |
| Uratibu Na Udhibiti Wa Dawa Za Kulevya | 6. Ujenzi Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni | Kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya shilingi TZS. 2,684,942,932.72 zilitumika kujengea kituo | SMZ | Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya |

| Sekta | Jina la Mradi | Thamani | Chanzo | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| | | hicho | | |
| Watu Wenye Ulemavu | 7. Ujumuishwaji wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar | Jumla ya shilingi TZS 46,220,000 zimepatikana | UNFPA | Idara ya Watu Wenye Ulemavu |
| Afya | 8. Afya ya Uzazi | 201,335,324 (shilingi) | Washirika wa Maendeleo | Tume ya UKIMWI |
| Afya | 9. Mapambano dhidi ya UKIMWI na Kifua Kikuu | Jumla ya shilingi TZS 126,573,000 zimepatikana | Washirika wa Maendeleo | Tume ya UKIMWI |

**Kiambatanisho nam. 5: Maeneo Yaliofanyiwa Ufuatiliaji wa Kimazingira**

| Nam. | Eneo | Idadi |
|---|---|---|
| | **(a) Unguja** | |
| i. | Kwa Mchina – Kukusanya na Kuchakata Plastiki | 2 |
| ii. | Chukwani – Kukusanya – vyuma chakavu, kuchakata – plastiki | 2 |
| iii. | Chunga – Kukusanya na kuokota – plastiki, kukusanya vyuma chakavu | 2 |
| iv. | Taveta – Kukusanya – vyuma chakavu | 2 |
| v. | Ijitimai – Kukusanya – vyuma chakavu | 1 |
| vi. | Kisauni – Kukusanya na kuchakata – vyuma chakavu | 1 |
| vii. | Kiembe Samaki – Kukusanya – vyuma chakavu | 1 |
| viii. | Kinuni | 1 |
| ix. | Magogoni | 2 |
| x. | Mnarani Fuoni | 1 |
| xi. | Donge – Chelele – Uchimbaji wa mchanga | 1 |
| xii. | Jendele – Uchimbaji wa kifusi | 1 |
| | | |
| | **Jumla Unguja** | **17** |
| | **(b) PEMBA** | |
| i. | Ole Finya – Shimo la mchanga la Serikali | 1 |
| ii. | Ole Bomani – Wizi wa mchanga | 1 |
| iii. | Ole - Kengeja na Mangwena – Urejeshwaji wa maeneo yaliojengwa Daraja | 1 |
| iv. | Vitongoji Makaani – Uchimbaji wa kokoto | 1 |
| v. | Pujini kwareni- Uchimbaji kifusi | 1 |
| vi. | Hospital ya Mkoani - Insenarator ya kuchomea | 1 |
| | taka | |
| vii. | Mwambe - Kware ya kifusi. | 1 |
| viii. | Pujini - Kware ya Kifusi | 1 |
| ix. | Vitongoji - Jaa kuu la Baraza la Mji Chake Chake | 1 |

| | | |
|---|---|---|
| x. | Mikindani Tungamaa - Jaa kuu la Baraza la Mji Wete | 1 |
| xi. | Chokaani - Jaa la kuu la Baraza la Mji Mkoani | 1 |
| xii. | Shumba - Shimo la Mchanga | 1 |
| | **Jumla Pemba** | **12** |
| | **Jumla kuu (Unguja + Pemba)** | **29** |

**Kiambatanisho nam. 6: Miradi Iliyofanyiwa Tathmini za Kimazingira**

| | |
|---|---|
| a) | Miradi iliyofanyiwa Tathmini za Athari za Kimazingira (Environmental Impact Assessment – EIA) |
| 1. | Ujenzi wa Hoteli ya Seven diamond, Nungwi, Wilaya ya Kaskazini 'A'. |
| 2. | Mradi wa Uendelezaji wa eneo la Michenzani (Intergrated Redevelopment project Michenzeni green corridor plan), Wilaya ya Mjini, Unguja |
| 3. | Ujenzi wa Hoteli ya F Zeen Beach Resort at Kizimkazi, Wilaya ya Kusini |
| 4. | Ujenzi wa mradi wa Jetty ya Hotel ya Blue Moon Resort Kajengwa, Wilaya ya Kusini |
| 5. | Ujenzi wa mradi wa Pier/wharf Structure Malindi Wilaya ya Mjini |
| 6. | Ujenzi wa Bandari ya KMKM iliopo Kibweni Wilaya ya Magharibi 'A' |
| 7. | Ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu, Wilaya ya Kati |
| 8. | Ujenzi wa Mtambo wa kuchoma taka hatarishi za hospitali (Biohazardous waste management plant) kiliopo Marumbi, Wilaya ya Kati |
| 9. | Ujenzi wa Jeti ya mradi wa hoteli ya Residential villa iliopo Jambiani Mfumbwi, Wilaya ya Kusini Unguja |
| 10. | Ujenzi wa kiwanda cha kukaushia dagaa (ZAFICO -Anchovy Processing Unit) kiliopo Fungu refu Mto wa pwani, Wilaya ya Kaskazini A |
| 11. | Ujenzi wa mradi wa hoteli ya Barefoot resort iliopo Msitu wa Hifadhi wa Ras kiuyu, Micheweni, Wilaya ya Kaskazini Pemba |

**Kiambatanisho nam. 6: Miradi Iliyofanyiwa Tathmini za Kimazingira**

| |
|---|
| 12. Ujenzi wa mradi wa hoteli ya Pilipili Natural Park iliopo Dongwe Bwejuu, Wilaya ya Kusini |
| 13. Ujenzi wa hoteli ya Crown iliopo Mazizini, Wilaya ya Magharibi 'B'. |
| 14. Ujenzi wa mradi wa hoteli ya Bamboo Beach Resort, iliopo Jambiani Kikadini, Wilaya ya Kusini |
| 15. Ujenzi wa mradi wa Hoteli ya Senxation Beach Villa Resort iliopo Makangale Micheweni Wilaya ya Kaskazini Pemba |
| 16. Ujenzi wa mradi wa hoteli wa Riu Jambo Hotel and Resort iliopo Kendwa, Wilaya ya Kaskazini A |
| 17. Ujenzi wa mradi wa hoteli ya Stay Zanzibar Resort iliopo Pongwe Pwani, Wilaya ya Kati |
| 18. Ujenzi wa mradi wa hoteli ya Tembo Kiwengwa Beach Resort iliopo Kiwengwa, Wilaya ya Kaskazini 'B'. |
| 19. Ujenzi wa mnara wa mawasiliano (Telecommunication tower znz 080) uliopo Fuoni Mambosasa, Wilaya ya Magharibi 'B' |
| 20. Ujenzi wa mnara wa mawasiliano (Telecommunication tower znz 052) Uliopo Tumbatu Jongowe, Wilaya ya Kaskazini 'A' |
| 21. Ujenzi wa mnara wa mawasiliano (Telecommunication tower znz 050) uliopo Kisiwa cha Uzi, Wilaya ya Kati |
| 22. Ujenzi wa mnara wa mawasiliano (Telecommunication tower znz 054) uliopo Bumbwini Makoba, Wilaya ya Kaskazini 'B' |
| 23. Ujenzi wa mnara wa mawasiliano (Telecommunication tower znz 049) uliopo Kama, Wilaya ya Magharibi 'A' |
| 24. Ujenzi wa mnara wa mawasiliano (Telecommunication tower znz 047) uliopo Maziwa Ng'ombe Pemba |

**Kiambatanisho nam. 6: Miradi Iliyofanyiwa Tathmini za Kimazingira**

| | |
|---|---|
| 25. | Ujenzi wa mnara wa mawasiliano (Telecommunication tower znz 044) uliopo Kisiwani Pemba |
| 26. | Ujenzi wa mnara wa mawasiliano (Telecommunication tower znz 043) uliopo Chambani Pemba |
| 27. | Ujenzi wa mrdi wa hoteli ya Soft Sand Resort iliopo Jambiani, Wilaya ya Kusini, Unguja |
| 28. | Ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua (intergraded Drainage and Resilient Urban Upgrading) uliopo Mkoa wa Mjini Magharibi |
| b) | Miradi iliyofanyiwa ukaguzi wa kimazingira |
| 1. | Mradi wa hoteli ya Nungwi Dream Resort iliopo Nungwi, Wilaya ya Kaskazini 'A' |
| 2. | Mradi wa hoteli ya Zanzibar Serena iliopo Shangani, Wilaya ya Mjini |
| 3. | Mradi wa hoteli ya Zanzibar Beach Resort iliopo Mazizini, Wilaya ya Magharibi 'B' |
| 4. | Mradi wa mnara wa mawasiliano (ID ZAN 014) uliopo Fuoni (telecommunication tower D ZAN 952) uliopo Fuoni Chunga |
| 5. | Mradi wa minara ya mawasiliano (Telecommunication tower (IDZAN 016) Tunguu, (ID ZAN 018) Machui, (ID ZAN 020) Chwaka na (ID ZAN 021) Jambiani |
| 6. | Mradi wa minara ya mawasiliano (telecommunication tower (ID ZAN 001) Mji Mkongwe, (ID ZAN 017) Maruhubi na (ID ZAN 021) Meya |
| 7. | Mradi wa minara ya mawasiliano (telecommunication tower) (ID ZAN 007) Nungwi, (ID ZAN 015) Mahonda, (ID ZAN 019) Mkwajuni na (ID ZAN 024) Kinyasini |

**Kiambatanisho nam. 6: Miradi Iliyofanyiwa Tathmini za Kimazingira**

| | |
|---|---|
| c) | Miradi iliandaliwa Ripoti za Kimazingira |
| 1. | Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta (Nifty filling station) kiliopo Binguni, Wilaya ya Kati |
| 2. | Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta kiliopo Mkanyageni Wilaya ya Magharibi 'A' |
| 3. | Mradi wa ujenzi wa Jetty ya Kisiwa cha Niamembe kiliopo Wilaya ya Kati |
| 4. | Mradi wa ujenzi wa hoteli ya Complex hotel iliopo Paje, Wilaya ya Kusini |
| 5. | Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta kiliopo (Nifty filling station) kiliopo Jumbi, Wilaya ya Kati |
| 6. | Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta kiliopo Kilindi- Kendwa, Wilaya ya Kaskazini 'A' |
| 7. | Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Nishati ya Jua (solar power PV plant) kiliopo Bwejuu, Wilaya ya Kusini |
| 8. | Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta (Classic petrol station) kiliopo Wawi, Wilaya ya Chake Chake Pemba |
| 9. | Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta (Mtuhaliwa Petrol Station) kiliopo Mtuhaliwa, Mkoani Pemba. |
| 10. | Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta (Mzambarautakao Petrol Station) kiliopo Mzambarautakao, Wilaya ya Wete |
| 11. | Mradi wa ujenzi wa hoteli ya SKY2 fox iliopo Kizimkazi Mkunguni, Wilaya ya Kusini |
| 12. | Mradi wa ujenzi wa nyumba (Private Farm Villa) iliopo Jambiani Mfumbwi, Wilaya ya Kusini. |

**Kiambatanisho nam. 6: Miradi Iliyofanyiwa Tathmini za Kimazingira**

| |
|---|
| 13. Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta (Bwejuu Mzambarauni Petrol Station) kiliopo Bwejuu, Wilaya ya Kusini. |
| 14. Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta (Nuru Petrol Station) kiliopo Matemwe Mbuyu Tende, Wilaya ya Kaskazini 'A'. |
| 15. Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Coral and Spa iliopo Jambiani Kikadini, Wilaya ya Kusini. |
| 16. Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta (12 Kikosi cha Jeshi Filling Station) kiliopo Migombani, Wilaya ya Mjini. |
| 17. Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Nishati ya Jua (Solar Power PV Plant) kiliopo Fumba, Wilaya ya Magharibi 'B'. |
| 18. Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Villa Unaweza iliopo Matemwe, Wilaya ya Kaskazini 'A'. |
| 19. Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Agua Beach Resort iliopo Bwejuu, Wilaya ya Kusini. |
| 20. Mradi wa ujenzi wa workshop ya Chako (Chako Zanzibar Upcycled) iliopo Mbuzini, Wilaya ya Magharibi 'A'. |
| 21. Mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Maisha iliopo Nungwi, Wilaya ya Kaskazini 'A'. |
| 22. Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta (Kivunge Petrol Station) kiliopo Kivunge, Wilaya ya Kaskazini 'A'. |

**Kiambatanisho nam. 7: Miradi ya Kiuchumi na Kimaendeleo Iliyofanyiwa Ufuatiliaji wa Kimazingira**

| **(a) Unguja** |
|---|
| 1. Hoteli ya Esque ZALU Zanzibar - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 2. Hoteli ya Zanzibari Boutique - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 3. Hoteli ya Tanzanite - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 4. Nyumba ya Kulaza Wageni ya Makofi (Makofi guest house) - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 5. Hoteli ya Nungwi Getway - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 6. Hoteli ya Kihori (Kihori Bungalows) - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 7. Hoteli ya Amani (Amani Bungalow) - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 8. Hoteli ya Z (Z hotel) - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 9. Hoteli ya Double trees - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 10. Hoteli ya Sun Set (Sun Set Resort) - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 11. Hoteli ya Palumbo (Palumbo Beach) - Kendwa, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |

**Kiambatanisho nam. 7: Miradi ya Kiuchumi na Kimaendeleo Iliyofanyiwa Ufuatiliaji wa Kimazingira**

| |
|---|
| 12. Hoteli ya Mocco (Mocco Beach Villa) - Kendwa, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 13. Hoteli ya Parachichi – Kendwa, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 14. Hoteli ya Amani (Amani Kendwa Beach Resort) – Kendwa, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 15. Hoteli ya Baraka (Baraka Beach Bungalow) - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 16. Hoteli ya Almasi (Almasi Beach Resort) - Nungwi, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 17. Hoteli ya Kena (Kena Beach Hotel) - Matemwe, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 18. Hoteli ya Zanzibar queen unique (Zanzibar Queen Unique hotel) - Matemwe, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 19. Hoteli ya Zanzibar pearl - Matemwe, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 20. Hoteli ya Seles (Seles Bungalow) - Matemwe, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 21. Hoteli ya Villa Kiva - Matemwe, Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Unguja |
| 22. Mradi wa Nyumba za Nyamanzi (Fumba Town Development) – Nyamanzi, Wilaya ya Magharibi ‘B’, Unguja |

**Kiambatanisho nam. 7: Miradi ya Kiuchumi na Kimaendeleo Iliyofanyiwa Ufuatiliaji wa Kimazingira**

| |
|---|
| 23. Hoteli ya Sunshine (Sunshine Hotel) - Matemwe, Wilaya ya Kaskazini 'A', Unguja |
| 24. Hoteli ya Karafuu (Karafuu Hotel) - Michamvi, Wilaya ya Kusini, Unguja |
| 25. Hoteli ya Asilia (Asilia Retreat Villa) - Matemwe, Wilaya ya Kaskazini 'A', Unguja |
| **(b) Pemba** |
| 1. Hoteli ya Mantareef (Mantareef Hotel) - Makangale |
| 2. Mradi wa Swahili Divers (Swahili Divers) - Makangale |
| 3. Mradi Afro - Diver - Makangale |
| 4. Hoteli ya Emarald (Emarald Guest House) - Chokocho |
| 5. Hoteli IANA (IANA Hotel) - Makangale |
| 6. Hoteli ya Fundu Lagoon (Fundu Lagoon) - Wambaa |
| 7. Hoteli ya Misali Sunset Beach (Misali Sunset Beach) - Wesha |
| 8. Mradi wa Oxygen Holding - Mtambwe |
| 9. Mradi wa Kituo cha Mafuta cha Ntuhaliwa (Ntuhaliwa Petrol Station) - Ntuhaliwa |
| 10. Mradi wa Kituo cha Mafuta cha Limbani (Limbani Petrol Station) - Limbani |

**Kiambatanisho nam. 7: Miradi ya Kiuchumi na Kimaendeleo Iliyofanyiwa Ufuatiliaji wa Kimazingira**

| |
|---|
| 11. Mradi wa Kipapo Mgelema & Kisiwani Birikau Road Construction |
| 12. Barabara ya Kipapo – Mgelema. |
| 13. Barabara ya Kisiwani Wesha – Birikau. |
| 14. Barabara ya maeneo huru Maziwa Ng'ombe. |

**Kiambatanisho Nam. 8: Taarifa za Malalamiko ya Kimazingira Zilizopokelewa na Kushughulikiwa**

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
|---|---|---|
| **1.** Kiwanja cha Mpira cha Timu ya Mwembeladu kilichopo Sebleni kwa wazee. | Uchimbaji mchanga, utupaji taka ovyo, kulaza magari na kupanda migomba. | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 02/09/2020 ambapo walikubaliana na wananchi wa eneo hilo walisafishe eneo, waing'owe migomba iliyokuwemo, waondoshe magari yao pamoja na kusafisha taka na kuzuia kuchota mchanga jukumu hili walikabidhiwa Manispaa ya Mjini pamoja na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, na jukumu la kusawazisha uwanja ambalo walikabidhiwa mradi wa ZUSP ambao walikuwa wakilitumia kwa shughuli zao. |
| 2. Fuoni Mambosasa | Kudidimia kwa nyumba kufuatia mvua kubwa zilizonyesha | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 07/09/2020 ambapo ilikubaliwa kutoa taarifa kwa wakaazi wa eneo hilo kuwa eneo hilo lipo katika hatari na linaweza kusababisha maafa, eneo lipimwe na liwekwe katika orodha ya maeneo hatarishi |
| 3. Mwanakwerekwe | Kelele, moshi wa vigae na Utiririshaji wa maji machafu unaofanywa na kiwanda cha kusaga chupa | ZEMA iliandaa ziara ya wadau iliyofanyika tarehe 08/09/2020 ambapo mhusika amepewa muda hadi tarehe 31 Januari 2021 awe ameshahama na katika kipindi chote cha mpito hadi atakapohama anatakiwa kupunguza kelele, moshi na kuongeza mashirikiano na jamii wa eneo husika. |

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 4. Mwanakwerekwe Sokoni | Utupaji wa Taka ovyo | ZEMA iliandaa ziara ya wadau iliyofanyika tarehe 08/10/2020 ambapo ilikubaliwa kuwa Manispaa ya Magharibi 'B' kwa kushirikiana na Mkuu wa Soko la Mwanakwerekwe kusafisha na kuondoa jaa hilo. |
| 5. Mtoni Chemchem | Uchimbaji holela wa kifusi | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 26/11/2020 ambapo wananchi wa nyumba 3 walihamishwa kwa ajili ya kulinda afya na usalama wao kutokana na tishio la nyumba zao kudidimia. Wajumbe wa ziara walikubaliana kuwa wananchi hao wasiruhusiwe kurudi kwenye nyumba hizo, kujengwa uzio na kutoa elimu ya mazingira. |
| 6. Bwejuu | Utupaji wa taka | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 16/12/2020 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kusini ilitakiwa kutafuta eneo la kutupa taka kwa wakaazi wa Bwejuu ili kuondoa tatizo la utupaji taka ovyo kwenye fukwe za Bahari. |
| 7. Kwarara | Uharibifu wa mazingira unaoweza kupelekea maradhi ya mripuko | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 16/12/2020. Ambapo ilikubaliwa kuwa na ufuatiliaji mzuri ili kuhakikisha kuwa eneo hilo halirejei kutupwa taka ili kulinda afya za jamii, pia kufanya doria za usiku ili kudhibiti uchimbaji wa mchanga katika eneo hilo pamoja na kutoa elimu ya mazingira na usimamizi wa maliasili zisizorejesheka. |

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
| --- | --- | --- |
| 8. Kisiwani Shehia ya Wesha. | Kuweka udongo katika mikandaa | ZEMA ilifanya ziara katika husika tarehe 20/08/2020 ambayo ilipelekea udongo wote kuondolewa katika eneo hilo na eneo limeendelea kuwa kama lilivyokuwa awali, |
| 9. Makaani Shehia ya Vitongoji | Usumbufu wa nzi ambao wanafika maeneo yote ya makaani. | ZEMA ilifanya ziara katika eneo husika tarehe 23/09/2020 na kulitaka Baraza la Mji Chake Chake kuimarisha usimamizi bora wa jaa la Vitongoji. |
| 10. Kilima Hodi shehia ya mfikiwa | Ukataji wa mlima wa fuwe katika eneo ambalo lina mgogoro wa mpaka. | Tarehe 25/11/2020 Tulitembelea eneo hilo na watu wa misitu, kutoa tamko la kuzuia na baadae kumshauri DC akutane na wahusika ili kutatua mzozo huo kuepusha shari. |
| 11. Kisiwa cha Uzi Eneo la Nyeke, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Ukataji wa Mikoko Kinyume na Sheria | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 08/01/2021 na kupendekeza kutoa elimu kwa wananchi wa Kisiwa cha Uzi kuhusu umuhimu wa kutunza Mikoko, kufanya ufuatiliaji wa kimazingira katika maeneo hayo ili kuendeleza utunzaji wa Mikoko na kuhamasisha wananchi kutoa ushirikiano katika ulinzi na utunzaji wa Mikoko |
| 12. Vitongoji, Wilaya ya Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba. | Uchimbaji mchanga katika shamba | ZEMA kupitia kikosi cha doria kilifanya ziara ya kukagua eneo hilo na kujionea hali halisi na kukubaliana kuzidisha doria hasa wakati wa usiku ili kuwakamata wanaofanya uharibifu huo. |

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 13. Pongwe Pwani, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Ujenzi wa Hoteli katika eneo la Fukwe | ZEMA iliandaa ziara ya kukagua eneo hilo tarehe 02/02/2021 ambapo walikubaliana kusitisha ujenzi katika eneo hilo hadi atakapopata kibali maalum cha kutumia eneo hilo la fukwe. |
| 14. Mtoni chemchem , Wilaya ya Magharibi 'A' Mkoa wa Mjini Magharibi. | Uchimbaji wa Mchanga Kinyume na utaratibu | ZEMA kupitia kikosi cha Doria kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walifanya operesheni tarehe 03/02/2021 na kufanikiwa kuukamata mchanga tani 30 na kuutaifisha. |
| 15. Maungani, Wilaya ya Magharibi 'B', Mkoa wa Mjini Magharibi. | Uchimbaji wa mchanga kinyume na sheria | ZEMA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi waliandaa doria iliyofanyika tarehe 04/02/2021 ya kufanya ukaguzi wa eneo lililoathirika kwa uchimbaji mchanga kinyume na utaratibu na kujua hali halisi na kukubaliana kuongeza doria hasa katika nyakati za usiku na alfajiri ili kuwakamata wahusika wa uchimbaji wa mchanga |
| 16. Uroa pongwe, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Uchimbaji wa mchanga wa pwani kinyume na sheria | ZEMA iliandaa ziara ya wadau iliyofanyika tarehe 12/02/2021 na kuona hali halisi ya eneo na kupendekeza utoaji wa elimu kwa wakaazi wote wa Uroa-Pongwe kuhusiana na umuhimu wa kudhibiti mchanga huo pamoja na madhara ya kuchimba mchanga wa pwani na kuzidisha nguvu za doria hasa kwa nyakati za usiku na alfajiri. |

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 17. Uroa, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji ya bahari yasiende kwenye Madrasa | ZEMA ilifanya ziara ya wadau tarehe 17/02/2021 ili kujionea hali halisi pamoja na kuwataka wamiliki wa madrasa kufuata muongozo wa ujenzi wa ukuta huo wa kitaalamu pamoja na kushirikiana na majirani zake kujenga ukuta wa pamoja ambao utanusuru eneo lote hilo kuendelea kuathirika na maji ya bahari. |
| 18. Mwera Pongwe, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Kiwanda cha kokoto kinachosababisha kero kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya kiwanda | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 03/03/2021 na kumtaka mmiliki wa kiwanda kufuatilia kibali cha mazingira, pamoja na kuzingatia maagizo yaliyotolewa na Mkuu wa wilaya ya Kati ikiwemo kufanya kupunguza muda wa kufanya kazi ili kuondoa kero kwa wanaozunguka eneo la kiwanda |
| 19. Bweleo, Wilaya ya Magharibi 'B'. Mkoa wa Mjini Magharibi | Ujenzi wa kiwanda cha kutengenezea nyaya za umeme bila ya kuwa na vibali | ZEMA kwa kushirikiana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais walifanya ziara ya ukaguzi wa eneo husika tarehe 09/03/2021 na kusitisha ujenzi wa eneo husika mpaka vitakapopatikana vibali halali vya kutumia eneo hilo. |
| 20. Fuoni Kibonde Mzungu, Wilaya ya Magharibi 'B', Mkoa wa Mjini Magharibi | Kujaa maji ya mvua katika nyumba za wananchi | ZEMA ilifanya ziara ya wadau tarehe 10/03/2021 ili kujionea hali halisi ya eneo husika na kupata mapendekezo ya hatua muafaka za kuchukua |

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 21. Matemwe, Wilaya ya Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini Unguja. | Ujenzi wa ukuta wa kingo kwa kuzuia maji ya bahari. | ZEMA ilifanya ziara ya wadau tarehe 10/03/2021 ili kujionea hali halisi pamoja na kumtaka mmiliki afate taratibu za kutafuta vibali kwa mradi wake wa mkahawa pamoja na kumuomba awasilishe mchoro wa ukuta ambao anataka kujenga kwa kupata ushauri wa kitaalamu juu ya ujenzi wa ukuta huo |
| 22. Kisiwa cha Uzi Eneo la Nyeke, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Ukataji wa Mikoko Kinyume na Sheria | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 08/01/2021 na kupendekeza kutoa elimu kwa wananchi wa Kisiwa cha Uzi kuhusu umuhimu wa kutunza mikoko, kufanya ufuatiliaji wa kimazingira katika maeneo hayo ili kuendeleza utunzaji wa mikoko na kuhamasisha wananchi kutoa ushirikiano katika ulinzi na utunzaji wa Mikoko |
| 23. Vitongoji, Wilaya ya Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba. | Uchimbaji mchanga katika shamba | ZEMA kupitia kikosi cha doria kilifanya ziara ya kukagua eneo hilo na kujionea hali halisi na kukubaliana kuzidisha doria hasa wakati wa usiku ili kuwakamata wanaofanya uharibifu huo. |
| 24. Pongwe Pwani, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Ujenzi wa Hoteli katika eneo la Fukwe | ZEMA iliandaa ziara ya kukagua eneo hilo tarehe 02/02/2021 ambapo walikubaliana kusitisha ujenzi katika eneo hilo hadi atakapopata kibali maalum cha kutumia eneo hilo la fukwe. |

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 25. Mtoni chemchem , Wilaya ya Magharibi 'A' Mkoa wa Mjini Magharibi. | Uchimbaji wa Mchanga kinyume na utaratibu | ZEMA kupitia kikosi cha Doria kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walifanya operesheni tarehe 03/02/2021 na kuukamata mchanga tani 30 na kuutaifisha. |
| 26. Maungani, Wilaya ya Magharibi 'B', Mkoa wa Mjini Magharibi. | Uchimbaji wa mchanga kinyume na sheria | ZEMA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi waliandaa doria iliyofanyika tarehe 04/02/2021 ya kufanya ukaguzi wa eneo lililoathirika kwa uchimbaji mchanga kinyume na utaratibu na kujua hali halisi na kukubaliana kuongeza doria hasa katika nyakati za usiku na alfajiri ili kuwakamata wahusika wa uchimbaji wa mchanga |
| 27. Uroa pongwe, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Uchimbaji wa mchanga wa pwani kinyume na sheria | ZEMA iliandaa ziara ya wadau iliyofanyika tarehe 12/02/2021 na kuona hali halisi ya eneo na kupendekeza utoaji wa elimu kwa wakaazi wote wa Uroa-Pongwe kuhusiana na umuhimu wa kudhibiti mchanga huo pamoja na madhara ya kuchimba mchanga wa pwani na kuzidisha nguvu za doria hasa kwa nyakati za usiku na alfajiri. |
| 28. Uroa, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji ya bahari yasiende kwenye Madrasa. | ZEMA ilifanya ziara ya wadau tarehe 17/02/2021 ili kujionea hali halisi pamoja na kuwataka wamiliki wa madrasa kufuata muongozo wa ujenzi wa ukuta huo wa kitaalamu pamoja na kushirikiana na majirani zake kujenga ukuta wa pamoja |

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | ambao utanusuru eneo lote hilo kuendelea kuathirika na maji ya bahari. |
| 29. Mtoni, Wilaya ya Magharibi 'A', Mkoa wa Mjini Magharibi | Ukataji wa meli chakavu bila ya kibali | ZEMA ilifanya ziara tarehe 01/03/2021 katika eneo ambalo linakatwa meli ya MV HASANATI na kuona hali halisi iliyopo pamoja na kusitisha shughuli hiyo mpaka atakapofanya taratibu zote husika za kupata kibali kitakachowaruhusu kukata meli hiyo. |
| 30. Mwera Pongwe, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja | Kiwanda cha kokoto kinachosababisha kero kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya kiwanda | ZEMA iliandaa ziara ya wadau tarehe 03/03/2021 na kumtaka mmiliki wa kiwanda kufuatilia kibali cha mazingira, pamoja na kuzingatia maagizo yaliyotolewa na Mkuu wa wilaya ya Kati ikiwemo kufanya kupunguza muda wa kufanya kazi ili kuondoa kero kwa wanaozunguka eneo la kiwanda |
| 31. Bweleo, Wilaya ya Magharibi 'B'. Mkoa wa Mjini Magharibi | Ujenzi wa kiwanda cha kutengenezea nyaya za umeme bila ya kuwa na vibali | ZEMA kwa kushirikiana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais walifanya ziara ya ukaguzi wa eneo husika tarehe 09/03/2021 na kusitisha ujenzi wa eneo husika mpaka vitakapopatikana vibali halali vya kutumia eneo hilo. |
| 32. Fuoni Kibonde Mzungu, Wilaya ya Magharibi 'B', Mkoa wa Mjini Magharibi | Kujaa maji ya mvua katika nyumba za wananchi | ZEMA ilifanya ziara ya wadau tarehe 10/03/2021 ili kujionea hali halisi ya eneo husika na kupata mapendekezo ya hatua muafaka za kuchukua |

| Shehia/Eneo | Hoja | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 33. Matemwe, Wilaya ya Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini Unguja. | Ujenzi wa ukuta wa kingo kwa kuzuia maji ya bahari. | ZEMA ilifanya ziara ya wadau tarehe 10/03/2021 ili kujionea hali halisi pamoja na kumtaka mmiliki afuate taratibu za kutafuta vibali kwa mradi wake wa mkahawa pamoja na kumuomba awasilishe mchoro wa ukuta ambao anataka kujenga kwa kupata ushauri wa kitaalamu juu ya ujenzi wa ukuta huo. |

**Kiambatanisho Nam. 9: Idadi na Aina ya Vipindi vya Redio na TV vilivyotayarishwa na kurushwa hewani**

| Namb | Aina ya Kipindi | Aina ya Redio/TV |
|---|---|---|
| **Vipindi vya Redio** | | |
| 1. | Athari za mifuko ya plastiki kwa ardhi ya kilimo na Wanyama | Redio Jamii Mkoani |
| 2. | Ushiriki wa Wanafunzi katika Vilabu vya Mazingira Maskulini | ZBC |
| 3. | Umuhimu wa kupanda, kulinda na kuhifadhi mikoko | ZBC |
| **Vipindi vya TV** | | |
| 1. | Usafi wa Mazingira na Tahadhari za mvua | ZBC |
| 2. | Athari za uchimbaji holela wa mchanga na utaratibu w akufuata wa kuchimba mchanga kihalali | ZBC |

| Namb | Aina ya Kipindi | Aina ya Redio/TV |
|---|---|---|
| 3. | Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mfumo wa Ekolojia vijijini | ZBC |
| 4. | Athari ya Mabadiliko ya Tabianchi katika sekta ya kilimo | ZBC |

## Kiambatanisho Nam. 10: Mchanganuo wa Wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu

| | **Unguja** | | **Pemba** | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | ME | KE | |
| **Mikopo** | 30 | 17 | 22 | 10 | 79 |
| **Elimu** | 3 | 0 | 3 | 0 | 6 |
| **Matibabu** | 2 | 2 | 1 | 0 | 5 |
| **Jumla Kuu** | | | | | **93** |
| **Vikundi** | 3 | | 0 | | 3 |

## Kiambatanisho Nam. 11 Idadi ya Wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

| Fani za Watumishi | Sdt 1 - F.IV | | Cheti | | Stashahada | | Stashahada ya Juu | | Shahada ya Kwanza | | Stashahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamivu | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | |
| Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 17 | 7 | 0 | 3 | 1 | 11 | 0 | 1 | 6 | 5 | 0 | 0 | 5 | 4 | 0 | 0 | 60 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 8 |
| Idara ya Watu Wenye Ulemavu | 6 | 7 | 2 | 0 | 5 | 5 | 1 | 0 | 7 | 23 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 59 |
| Idara ya Mazingira (Unguja) | 4 | 3 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 1 | 3 | 9 | 1 | 0 | 4 | 4 | 0 | 0 | 34 |

## Kiambatanisho Nam. 11 Idadi ya Wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

| Fani za Watumishi | Sdt 1 - F.IV | | Cheti | | Stashahada | | Stashahada ya Juu | | Shahada ya Kwanza | | Stashahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamivu | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | |
| Idara ya Mazingira (Pemba) | 7 | 4 | 0 | 0 | 2 | 6 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 25 |
| Mamlaka ya Mazingira (Unguja) | 12 | 5 | 4 | 6 | 1 | 5 | 0 | 0 | 3 | 7 | 5 | 0 | 4 | 5 | 0 | 0 | 57 |
| Tume ya UKIMWI (Unguja) | 2 | 2 | 3 | 1 | 1 | 4 | 1 | 0 | 1 | 5 | 1 | 1 | 5 | 3 | 0 | 0 | 30 |
| Mamlaka ya Mazingira (Pemba) | 10 | 0 | 1 | 0 | 2 | 6 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 24 |
| Tume ya UKIMWI (Pemba) | 1 | 1 | 0 | 0 | 4 | 2 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 14 |

## Kiambatanisho Nam. 11 Idadi ya Wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

| Fani za Watumishi | Sdt 1 - F.IV | | Cheti | | Stashahada | | Stashahada ya Juu | | Shahada ya Kwanza | | Stashahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamili | | Shahada ya Uzamivu | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | *M* | *F* | |
| Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya (Unguja) | 7 | 1 | 2 | 1 | 1 | 7 | 1 | 0 | 2 | 10 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 34 |
| Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya (Pemba) | 0 | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| Ofisi Kuu Pemba | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 4 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 |
| **JUMLA** | **68** | **31** | **14** | **15** | **19** | **53** | **4** | **2** | **35** | **66** | **9** | **1** | **30** | **19** | **1** | **0** | **367** |

## Kiambatanisho Nam. 12: Stahiki za Wafanyakazi

| Idara/Taasisi | Stahiki za Likizo | | Stahiki za Saa baada ya Kazi | | Stahiki za Ufiwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Unguja** | **Pemba** | **Unguja** | **Pemba** | **Unguja** | **Pemba** | **Jumla** |
| Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 6 | 0 | 59 | 0 | 0 | 0 | 65 |
| Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 3 | 0 | 7 | 0 | 1 | | 11 |
| Idara ya Faragha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Idara ya Watu Wenye Ulemavu | 15 | 2 | 17 | 0 | 5 | 0 | 39 |
| Idara ya Mazingira | 10 | 6 | 21 | 0 | 2 | | 39 |
| Mamlaka ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira | 24 | 6 | 9 | 2 | 2 | 1 | 44 |
| Tume ya UKIMWI | 6 | 2 | 3 | 0 | 2 | 0 | 13 |
| Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar | 8 | 1 | 2 | 3 | 2 | 0 | 16 |
| Ofisi Kuu Pemba | 0 | 3 | 0 | 6 | 0 | 1 | 10 |
| **JUMLA** | **72** | **20** | **118** | **11** | **14** | **2** | **237** |

**Kimbatanisho Nam. 13: Idadi ya Watumishi Waliopatiwa Mafunzo**

| Idara/Taasisi | Mafunzo ya Muda Mrefu | | Mafunzo ya Muda Mfupi | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Unguja** | **Pemba** | **Unguja** | **Pemba** | **Jumla** |
| Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Idara ya Faragha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ofisi kuu Pemba | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Idara ya Watu Wenye Ulemavu | 7 | 0 | 1 | 0 | 8 |
| Idara ya Mazingira | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Mamlaka ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Tume ya UKIMWI | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| Tume ya Kitaifa Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar | 2 | 0 | 3 | 2 | 7 |
| **JUMLA** | **18** | **2** | **5** | **2** | **27** |






Ziara za Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya kusimamia Ofisi za Viongozi wakuu wa kitaifa katika maeneo yaliyopandwa mikoko kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi